Je, maneno:
as-Salaatu Khayrun Mina ‘n-Nawm
Ni Katika Maneno ya Adhana?

Kimeandikwa na:
Sayyid Abdur-Rahim al-Musawi

Kimetarjumiwa na:
Ustadh Abdallah Mohamed

© Haki ya kunakili imehifadhiwa na:
AL-ITRAH FOUNDATION

ISBN: 978 - 9987 - 427 - 57 - 4

Kimeandikwa na:
Sayyid Abdul Rahim al-Musawi

Kimetarjumiwa na:
Ustadh Abdallah Muhammad

Kimehaririwa na:
Sheikh Harun Pingili

Kupangwa katika Kompyuta na:
Ukhti Pili Rajab.

Toleo la kwanza: Machi, 2008
Nakala: 1000

Kimetolewa na kuchapishwa na:
Alitrah Foundation
P.O. Box 19701
Dar es Salaam, Tanzania
Simu:+255 22 2110640
Simu/Fax: +255 22 2127555
Email: alitrah@raha.com
Website: www.alitrah.org
Online: www.alitrah.info

YALIYOMO

1. Utangulizi.....2

2. Riwaya za adhana katika *Sahih* na *Musnad*.....*3*

3. Mosi: Mjadala juu ya riwaya za adhana zilizotangulia kutajwa sanad zake.....11

4. Njia ya pili: Namna riwaya hizo zilivyotaja namna ya kuwe kwa adhana kunaenda kinyume na misingi maarufu ya kuwekwa hukmu.....16

5. Tatu: Walioota ni watu kumi na wane na si mmoja pekee.....18

6. Nne: Kuna mgongano kati ya riwaya ya Bukhari na zingine.....19

7. Njia ya tano: Maoni ya wanavyuoni wa Shi'a juu ya kuongeza maneno kwenye adhana.....25

8. Njia ya Sita: Namna ya kuwekwa adhana kwa madhehebu ya Ahul bayt.....29

9. Muhtasari wa utafiti..... 39

NENO LA MCHAPISHAJI

Kitabu kilichoko mikononi mwako, ni tarjuma ya kitabu cha Kiarabu kwa jina la: "" kilichoandikwa na **Sayyid Abdul Rahim al-Musawi**
Sisi tumekiita: ""

Kitabu hiki kinazungumzia kuhusu Asili ya Adhana na jinsi ilivyokuja kwa Mtukufu Mtume. Kuna tofauti za kimapokezi kati ya madhehebu za Kiislamu, hususan Sunni na Shia. Na pia zipo hitilafu miongoni mwa wanachuo wenyewe kwa wenyewe ndani ya madhehebu za Kisunni kuhusu suala hili, kama utakavyoona katika kitabu hiki.

Kitu ambacho wamehitalafiana ni maneno: ***as-Salaatu Khayrun Mina 'n-Nawm*****,** kwamba ni maneno ya asili ya adhana au yaliongezwa na watu baada ya Mtukufu Mtume kuondoka? Hili ndio suala linalojadiliwa katika kitabu hiki.

Mwaandishi wa kitabu hiki amefanya utafiti wa hadithi na matukio ya kihistoria kuhusiana na suala hili, na kutokana na utafiti wake huo anaonesha kwa uwazi kabisa kwamba maneno: *Assalaatu khayrun mina'n-naumi,* yamekuja baada ya Mtukufu Mtume (s.a.w.) na kwamba hayana asili katika Adhana na kwamba maneno yenye asili katika Adhana ni: *hayya a'laa khayril-a'mal.*

Madhumuni ya kitabu hiki sio kuleta ugomvi au malumbano na wale wanao yakubali maneno: *Assalaatu khayrun mina'n-naumi,* bali ni kuwafahamisha wale wanaoshangaa wanapowasikia Waislamu wengine hawayaleti maneno haya katika Adhana yao na badala yake wanaleta maneno: *hayya a'laa khayril-a'mal.*

Taasisi yetu ya **'Al-Itrah Foundation'** imeona ikitoe kitabu hiki ili wasomaji wetu Waislamu wa Kiswahili waifahamu tofauti hii na waelewe maana yake na waondokane na dhana ziszokuwa na maana.

Tunamshukuru ndugu yetu, **Ust. Mohamed Abdallah** kwa kukubali jukumu hili la kukifanyia tarjuma kitabu hiki. Vilevile tunawashukuru wale wote walioshiriki kwa njia moja au nyingine hadi kufanikisha kuchapishwa kwa kitabu hiki.

Mchapishaji:
Al-Itrah Foundation
S. L. P. 19701
Dar-es-Salaam, Tanzania.

Utangulizi

Miongoni mwa maswala ambayo bado ni mahali pa tofauti baina ya madhehebu za kiislamu, ni suala la adhana na ibara zinazotamkwa ndani yake, kama vile ibara: **الصلاة خير من النوم** '*As-swalaatu khayrun minan nawm'* na huwezi ukafanya utafiti wa mas'ala haya bila ya kujua adhana ilivyowekwa kisheria. Rejea ya vyanzo vya Hadith kwa ma-Sunni inatufichulia idadi kadhaa – ya riwaya dhaifu na maqtu'u katika sanad zake, na zingine zaishilia kwenye hali ya kutojulikana, ambazo zatuambia jinsi adhana ilivyowekwa kisheria kupitia mtu mmoja aliyeota, bwana aitwaye Abdalla bin Zayd Al-Answari na Umar bin Al-Khattab, sababu ni kuwa Mtume (s.a.w.) alitaka ushauri juu ya adhana. Na zimekhitilafiana baadhi ya riwaya na zingine juu ya kwamba ibara: *as-swalatu khayrun minan nawmi* ilikuwa sehemu iliyoambatanishwa na kisa hiki kilichotokea wakati wa Mtume (s.a.w.), au mathalan, kuwa yeye (s.a.w) alimuamuru Bilal kutaja ibara hiyo badala ya kutaja **حي علي خير العمل** (*hayya a'laa khayril-a'mal*) ambayo imefutwa kwa masunni. Au ni kwamba Bilal aliitamka ibara hiyo na Mtume (s.a.w.) akaiwafiki. - Kuungana na ndoto au kuwa amri ya kuzidisha ni kutoka kwa Mtume (s.a.w) ilikuja wakati uliofuata.

Kama tulivyoona katika riwaya nyinginezo kwamba kutaja *as-Swallaat khayrun minan nawm* (Swala ni bora kuliko usingizi) kwamba ilikuwa ni katika ijtihadi ya Khalifa wa pili Umar bin Al-Khattab. Ama tukienda kwenye marejeo ya kisasa kwa wafuasi wa maimamu wa Ahlul-bayt tutaona kwamba aina ya adhana inahitilafiana na kijumla na kiufafanuzi na aina ya adhana kwa watu kwa kutegemea riwaya zilizopokewa na maimmu wa Ahlul-bayt, kutoka kwa babu yao Mtume (s.a.w.).

Riwaya za adhana katika *Sahih* na *Musnad*

Kabla ya kuingia kwa kina katika ufafanuzi wa masuala haya twaona ni bora kwanza tuonyeshe baadhi ya riwaya zenye kuhusika na tamko la *'swalaatu hayrun minan nawm'* pamoja na riwaya ambazo hazikutaja na ambazo zimenukuliwa na vitabu vya Sunni pamoja na sanad zao ili ifanye msingi na kigezo cha maongezi na darasa:
Ibn Maja: Ametuhadithia Muhammad bin Khalid bin Abdallah Al-Wasiti, amesema: Ametuhadithia baba yangu, kutoka kwa Abdur-Rahman bin Is'hak, kutoka kwa Zahri, kutoka kwa Salim, kutoka kwa baba yake, kwamba Mtume (s.a.w.) aliwashauri watu juu ya kitaka-chowahimiza kwenda kuswali.

Wakataja kuwekwe parapanda. Mtume (s.a.w.) hakupendelea hilo kwa kutumiwa na mayahudi. Wakataja kengele. Pia hakutaka kwa kuwa ilitumiwa na manaswara; kisha usiku huo, mtu mmoja katika ma-Answari, aitwaye Abdallah bin Zayd alionyeshwa ndotoni mwito huo na pia Umar bin Al-Khatab. Yule Ansari akamgongea mlango Mtume (s.a.w.) usiku, akamweleza, naye Mtume akamwamuru Bilal hivyo; naye akaadhini. Amesema Zahri: "Bilal akaongeza katika adhana ya alfajiri *(as-Swalatu khayrun minan nawmi)* Mtume (s.a.w.) akakubali kwa kuthibitisha.[1]

Amesema Abu Daud: "Ametuhadithia Musaddid, ametuhadithia Harth bin Ubayd kutoka kwa Muhammad bin Abdul-Malik bin Abi Mahdhurah, kutoka kwa babake, kutoka kwa babu yake, amesema: "Nilisema, ewe Mtume (s.a.w.) nifundishe Sunna ya adhana.

1. Sunnan Ibn Maja, Juz. 2. uk. 34. Kitabu cha Adhana, Mlango: Kuanza Adhana

Akasema: "akanigusa mbele ya kichwa changu akasema: "Utasema Allahu Akbar (mara nne) kisha utapaaza sauti yako useme: "Allahu Akbar" **الله اكبر** (mara nne), utapaaza sauti yako kisha useme, **آشْهَدُ اَنْ لاَ اِلـهَ اِلاَّ** Ash'hadu anlaa ilaaha illa'llah (mara mbili). Kisha useme:

اَشْهَدُ اَنّ مُحَمّدً رَسُولُ اللهِ Ash-hadu anna Muhammadan Rasulu'llah (mara mbili), kisha: **حَي على الصلاة :** hayya a'las-Swalaa (mara mbili), kisha **حَى على الْفَلاح** ' hayya a'lal'falaah (mara mbili), ikiwa ni Swala ya Al-fajiri useme, ' **الصلاة خير من النوم** as-Swalaatu khayrun minn nawm (mara mbili). Kisha useme:

الله اكْبَر الله اكْبَر لاَ اِلـهَ اِلاَّ الله: Allahu Akbar Allahu Akbar, laa ilaaha illa'llaah[2]

Na katika *Musnad* ya Ahmad, ametuhadithia baba yangu, kutoka kwa Is'hak, amesema: "Na ametaja Muhammad bin Muslim Az-Zahri, kutoka kwa Said bin Musayyib, kutoka kwa Abdallah bin Zaid bin Abdur-Rabbih, amesema: "Pindi Mtume (s.a.w.) alipoataka kuwakusanya watu kwa Swala kwa kutumia kengele, na alichukia kengele kwa kuwaafiki manaswara nilimuota mtu wakati nikiwa nimelala aliyevaa nguo za rangi ya kijani kibichi akiwa ameshikilia kengele mkononi mwake, nikamwambia ee mja wa Mwenyezi Mungu je wauza kengele? Akasema: "Kwani utaifanyia nini?" Nikasema, nitaitumia kukusanyia watu kwenye Swala. Akasema: "Je si nikuonyeshe kilicho bora zaidi ya hicho?" Nikaseama, ndio. Akasema: Useme, Allahu Akbar (mara nne), Ash-hadu anlaa ilaaha illa'llah (mara mbili), Ash-hadu anna Muhammadan Rasuuli llah (mara mbili), hayya a'las swalaa (mara mbili) hayya a'lal falaah (mara mbili), Allahu akbar (mara mbili), laa ilaaha illa llaah.

[2] *Sunna Abi Daud*; Kitabus swalaa, mlango wa namna ya adhana

Kisha akasema juu ya kukimu Swala: "Utasema, Allahu akbar (mara mbili), Ash-hadu anlaa ilaaha illa'llah (mara mbili), Ash-hadu anna Muhammadan Rasuuli'llah (mara mbili), hayya a'las swalaa (mara mbili) hayya a'lal falaah (mara mbili), Qad qaamatis swalaa (mara mbili), Allahu Akbar (mara mbili) laailaaha illa'llah. Akasema: "Kulipokucha nilikwenda kwa Mtume (s.a.w.).

Naye Mtume (s.a.w.) akasema: "Hakika ndoto hii ni ya kweli inshaallah" Kisha akaamuru kuadhiniwe. Akawa Bilal akiadhini hivyo na Mtume (s.a.w.) akilingania kwenye Swala. Anasema: Akaja akalingania usiku mmoja na akaambiwa kuwa Mtume (s.a.w.) alikuwa amelala, Bilal akapaaza sauti yake akisema: **الصلاة خير من النوم** 'As-swalaatu khayrun minan nawm'. Akasema Ibun Musayyib: "Ndipo neno hilo likaongezwa kwenye Swala ya Alfajiri."[3]

Katika *Sunan* ya Darmi: Ametuambia Uthman bin Umar bin Faris, ametuhadithia Yunus, kutoka kwa Zahri. Kutoka kwa Hafs bin Umar bin Saad - muadhini, ya kwamba Saad alikuwa akiadhini katika msikiti wa Mtume (s.a.w.)."

Amesema Hafs: "Amenihadithia ahli yangu kuwa Bilal alikwenda kuadhini kwa Mtume (s.a.w.) kwa ajili ya Swala ya Alfajiri. Wakamwambia kuwa Mtume (s.a.w.) amelala. Hapo Bilal akanadi kwa sauti yake kubwa, **الصلاة خير من النوم** 'As-swalaatu khayrun minan nawm', nayo ikathibitishwa hiyo katika adhana ya Swala ya Alfajiri.[4]

---

[3] *Musnad* ya Ahmad bin Hambal Juz. 4, uk. 632. Hadith ya Abdallah bin Zayd bin Asim Al-Mazini Hadith na. 16042

[4] *Sunnan Darmi*; Juz. 6, uk. 369 Hadith Na. 1192, langa wa tathwib fii adhanal fajri.

Katika *Majmauz-Zawaid*, ametuhadithia Ahmad bin Muhammad bin Al-Walid Al-Arzaqi, ametuambia Muslim bin Khalid, ametuhadithia Abdur-Rahim bin Umar, kutoka kwa Shihab, kutoka kwa Abdallah bin Umar kwamba Mtume (s.a.w.) alitaka kuweka kitu kitakachoweza kuwakusanya watu kwenye Swala, mpaka akaoteshwa mtu mmoja wa ki-Answari aitwaye Abdallah bin Zaid na pia akaoteshwa Umar bin Khattab usiku huo..mpaka aliposema: "Bilal akazidisha katika Swala ya Alfajiri kwa kusema **الصلاة خير من النوم** As-Swalaatu khayrun minan nawm. Na Mtume (s.a.w.) akaithibisha hiyo.[5]

Na kutoka kwa Bilal kwamba alikuwa akiadhini Swala ya Alfajiri akisema **حي علي خير العمل** *hayya a'laa khayril a'mal* ndipo Mtume (s.a.w.) akaamuru iwekwe mahali pake neno **الصلاة خير من النوم** *As-walaatu khayrun mina nawm* na aache neno **حي علي خير العمل** *hayya a'laa khayril a'mal.*[6]

Na imepokewa kutoka kwa Abu Huraira, amesema: "Alikwenda Bilal kwa Mtume (s.a.w.) ili aadhini kwa Swala ya Alfajiri, akasema: "Muamrisheni Abu Bakr aswalishe watu, akarudi kwake, akaona kwake uzito, akasema: "Muamrisheni Abu Bakr aswalishe watu. Akaenda akaadhini, na katika adhana akazidisha neno **الصلاة خير من النوم** '*As swalaatu khayrun minan nawm.*' Mtume (s.a.w.) akasema: Ni nini hii uliyozidisha katika adhana yako?" Akajibu: "Nimekuona una uzito nikataka kukuchangamsha." Mtume (s.a.w.) akasema: "Nenda kazidishe katika adhana yako na muamuru Abu Bakr aswalishe watu.[7]

---

5 *Tabaqaat* cha Ibn Saad Juz. 1 Uk. 247

6 *Majmauz-Zawa'id*, Juz. 1, uk. 33 Mlango wa namna ya kuadhini.

7 *Majmauz-Zawa'id*, Juz. 1, uk. 33 Mlango wa namna ya kuadhini.

9. Imepokewa kutoka kwa Abu Huraira kwamba Bilal alikwenda kwa Mtume (s.a.w.) wakati wa adhana ya Alfajiri. Akamkuta Mtume (s.a.w.) amelala, akamwita akisema: **الصلاة خير من النوم** *As-Swalaatu khayrun mina nnawm*' na Mtume (s.a.w.) hakumkataza na akaliingiza - yaani Bilal - neno hilo kwenye adhana, hivyo basi haiadhiniwi Swala kabla ya wakati wake isiokuwa Swala ya alfajiri.[8]

10. Imepokewa kutoka kwa Aisha amesema: "Alikwenda Bilal kwa Mtume (s.a.w.) ili amuadhinie kwa Swala ya Alfajiri, akamkuta amelala, akasema: **الصلاة خير من النوم** *As-Swalaatu khayrun minan nawm*; ikathibitishwa katika adhana ya asubuhi kuwa ndani ya adhana."[9]

Na katika *Sunnan Tirmidhi*, Hadith ya Ahmad bin Mu'in, ametuhadithia Abu Ahmad Zubeiry, ametuhadithia Abu Israil, kutoka kwa Hakam, kutoka kwa Abdul Rahman Abi Layla, kutoka kwa Bilal, amesema: "Ameniambia Mtume (s.a.w.) usiongeze kitu katika Swala ila katika Swala ya Al-fajiri."[10]

12. Amepokea Abu Daud amesema: "Ametuhadithia Ubbad bin Musa Al-Khatly, na Ziyad bin Ayyub, na Hadith ya Ziyad imetimia, wamesema wawili hao: "Ametuhadithia Hashim kutoka kwa Abu Bashar, amesema Ziyad: 'Ametuambia Abu Bashar, kutoka kwa Umayr bin Anas kutoka kwa maanswari amesema: "Mtume (s.a.w.) alikuwa na haja sana ya kufanya namna atakavyowakusanya waislamu kwa Swala. Akaambiwa, weka bendera wakati wa Swala unapoingia. Watu wakiiona wataambiana.

---

8 *Majmauz-Zawa'id*, Juz. 1, uk. 133, Mlango wa namna ya kuadhini.

9 *Majmauz-Zawa'id*, Juz. 1, jk. 33, Mlango wa namna ya kuadhini.

10 *Sunnan Tirmidhi*; Juz. 1, uk. 378, Hadith Na. 198

Hilo halikumpendeza. Akasema: "Akaambiwa apige parapanda (kama la Wayahudi), hilo pia halikumpendeza. Akasema: "Hiyo ni katika mambo ya Wayahudi." Akatajiwa kengele, akasema: "Hilo ni katika jambo la Manaswara."

Akaondoka Abdallah bin Zaid bin Abdur Rabbah, naye huyu akaoteshwa ndotoni adhana, akasema, akaenda mapema kwa Mtume (s.a.w.) na akampasha habari hiyo akisema: "Nilipokuwa katikati ya kulala na kuwa macho, mara alinijia mwenye kunijia na kunionyesha adhana. Amesema: "Na Umar bin Khattab alikuwa ameshaona kabla ya hapo na akalificha hilo kwa siku ishirini, kisha akamwambia Mtume (s.a.w.), naye akamwambia: "Nini kimekuzuia usinieleze?" Akajibu Umar: "Abdallah Bin Zaid alinitangulia hivyo nikaona haya kusema.

Hapo Mtume (s.a.w.) akasema: "Ee Bilal, simama na ufanye analokuamuru Abdallah bin Zaid." Akasema: "Akaadhini Bilal." Amesema Abu Bashar: "Akaniambia Abu Umayr kwamba Answari wanadai kuwa Abdallah bin Zaid lau asingelikuwa siku hizo ni mgonjwa, basi Mtume (s.a.w.) angelimfanya kuwa ni muadhini."[11]

13. Amesema: "Ametuhadithia Muhammad bin Mansur Tusi, ametuhadithia Yakub, ametuhadithia baba yangu, kutoka kwa Muhammad bin Is'hak, amenihadithia Muhammad bin Ibrahim bin Harith Taymi, kutoka kwa Muhammad bin Zaid bin Abdu Rabbih amesema: "Ametuhadithia Abdallah bin Zaid, amesema: "Mtume (s.a.w.) alipoamuru kengele ipigwe ili kukusanya watu kwa Swala, alikuja kwangu mtu, ilhali nimelala, akiwa na kengele mkononi, nikasema, ee Abu Abdallah je wauza kengele? Waifanyia nini? Nikajibu: "Tunaitia kwenye Swala.

11 *Sunnan Abu Daud*, Juz. 1, uk. 134, kitabu cha Swala, Mlango wa kuanza adhana

Akasema: "Je si nikuambie lililo bora zaidi kuliko hiyo kengele?" Nikamwambia, ndio niambie. Akasema: "Utasema, *Allahu Akbar* (mara nne); *Ashahdu*…. (mara mbili), *wa ash-hadu ana*…(mara mbili) hay'ya ala-Swalaa.(mara mbili) hay'ya alal falaah…(mara mbili) *Allah Akbar* (mara mbili) *laa ilaaha ila'llaah* (mara mbili). Akasema: kisha hakukawia sana akasema: "Na utapokimu Swala useme, *Allahu Akbar* (mara mbili), *Ash-hadu an'laaillaha ila'l-lah*….(mara moja), *wa ash-hadu ana*…(mara moja), *hay'ya ala swalaa* (mara moja) *hay'ya alal falaah…(*mara moja), *Qad qaamatis swalaa, qad qaamatis swalaa, Allahu akbar* (mara mbili), *laa ilaaha illa'llah*." Kulipokucha nilikwenda kwa Mtume (s.a.w.) nikamweleza niliyoyaona.

Naye akasema: "Hiyo ni ndoto ya kweli, inshaallah, simama na Bilal na umwambie uliyoyaona na aadhini kwayo, kwani yeye ana sauti kubwa zaidi kuliko wewe." Nikasimama na Bilal nikawa namsomea adhana hiyo. Akasema: Umar akasikia hilo akiwa nyumbani kwake akatoka huku akikokota nguo yake na akisema: "Naapa kwa yule aliyekutuma kwa haki! Ee Mtume (s.a.w.) wa Mwenyezi Mungu! Mimi pia nimeona hayo aliyoyaona." Mtume (s.a.w.) akasema: "Shukrani ni za Mwenyezi Mungu."

14. Amesema Ibn Maja: "Ametuhadithia Abu Bayd Muhammad bin Ubayd bin Maymuunul-Madani, amesema: "Ametuhadithia Muhammad bin Salama Al-Harani, amesema ametuhadithia Muhammad bin Is'hak, amesema, ametuhadithia Muhammad bin Ibrahim Taymi, kutoka kwa Muhammad bin Abdallah bin Zaid kutoka kwa baba yake, amesema: "Mtume (s.a.w.) alikuwa ana haja ya kutumia parapanda, akaambiwa atumie kengele, akakataa, hivyo Abdallah bin Zaid akaoteshwa usingizini."**12**

12 *Sunnan Ibn Maja*, Juz. 1, uk. 232

15. Na katika *Sunan Tirmidhi*: "Ametuhadithia Sa'ad bin Yahya bin Said Al-Amawi, ametuhaditha baba yangu, ametuhadithia Muhammad bin Is'hak, kutoka kwa Muhammad bin Ibrahim Taymi, kutoka kwa Muhammad bin Abdallah bin Zaid, kutoka kwa babake, amesema: "Kulipokucha, tulikwenda kwa Mtume (s.a.w.) na nikamwambia kuhusu hiyo ndoto…..Akasema Tirmidhi: "Amepokea Hadith hii Ibrahim bin Saad kutoka kwa Muhammad bin Is'hak, akakamilisha Hadith hii kwa urefu.

Kisha Tirmidhi akaongeza: "Na Abdallah bin Zaid naye ni Ibn Abdu Rabbih hatujui kwake Hadith ila hii pekee ya adhana."[13]

Kwa muhtasari, riwaya za Hadith hizi zina mambo yafuatayo:

Nyongeza ya ziyada ya maneno imekuja upande wa Bilal na Mtume (s.a.w.) akaithibitisha, na Abdallah bin Zaid hakuiona ndotoni wala Umar bin Al-Khattab kama vile riwaya za kuhusu adhana zilivyonukuu. Adhana Mtume (s.a.w.) alimfundisha Abi Mahdhur na ina neno **الصلاة خير من النوم** *As-Swaatu khayrun minnnawm*' ndipo likaingizwa kwenye adhana. Na katika riwaya nyingi, Bilal alipaaza sauti yake na huku Mtume (s.a.w.) akiwa amelala akasema,
الصلاة خير من النوم *As-Swalaatu khayrun minan-nawm'* ndipo neno hilo likingizwa kwenye adhana.

Na katika riwaya nyingine: Bilal alikuwa akiadhini kwa Swala ya Alfajiri akisema **حي علي خير العمل** *hay'ya a'laa khayril amal'* na hapo Mtume (s.a.w.) akaamuru neno hilo liwe badala ya neno **الصلاة خير من النوم** *As-Swalaatu khayrun mina-nawm.*'

Riwaya hizi zilizoandikwa na vitabu vya *Sunan* na ambazo zinataja

13 *Sunnan Tirmidhi*, Juz. 1, uk. 361 Mlango wa kuanza adhana. Na. 189

suala la neno *'As-swalaatu khayrun minan nawm'* katika adhana, na zingine hazikutaja, hizi hazizingatiwi, kwa sababu kadhaa zifuatazo: Kwanza, ni upande wa sanad, tunaona kuwa njia zake za upokezi, ama ni dhaifu ama ni zimekatika, ama hazijulikani.

Namna adhana ilivyowekwa kisheria inashangaza. Na hivyo ni kwa ajili ya kuwa kinyume na ile misingi ijulikanayo ya kuwekwa hukmu za kidini.

Kuwapo tofauti baina ya mafakihi wa kiislamu wa madhehebu manne katika suala la kuongeza neno - *Aswalatu khayrun minan-Nawmi* - katika adhana.

Mosi: Mjadala juu ya riwaya za adhana zilizotangulia kutajwa sanad zake:

Tutafafanua hapa zaidi kifungu hiki kuhusiana na sanad za riwaya na tutaangalia kulingana na mapokezi ya Hadith ya kwanza mpaka ya mwisho ili tuone katika hukmu kama ikiwa kutajwa **الصلاة خير من النوم** '*swalaatu khayrun minan nawm'* kulikuwapo wakati wa Mtume (s.a.w.) ama kulipendelewa baadaye na kuongezwa katika adhana kwa ijtihadi tu:

1. Muhammad bin Khalid bin Abdallah Al-Wasiti, Jamalud-Din Al-Mazzi anatoa taarifa yake akisema: "Amesema: "Ibn Mu'in hana kitu." Na riwaya yake kutoka kwa baba yake ilikanushwa.

Amesema Abu Hatim: "Nilimuuliza juu ya Yahya bin Mu'in, akasema: 'Huyo ni mtu muovu, muongo na ametaja mambo maovu." Na amesema Abu Uthman Said bin Umar na Bardai: "Nilimuuliza Aba Ara' juu ya Muhammad bin Khalid akasema huyo ni mtu muovu. Na Ibn Hayyan katika kitabu *At-Thuqaat*: akasema, huyo hukosa na

hukhalifu."[14]

Na Shawkani naye amesema baada ya kunakili riwaya: Kuwa katika isnadi yake kuna udhaifu sana.[15]

2. Dhahabi amesema: Muhammad bin Abdul Malik bin Abi Mahdhura, kutoka kwa baba yake kuhusu adhana kuwa siyo hoja.[16] Na katika kitabu *Naylul-awtaari* cha Shawkani imetajwa: Muhammad bin Abdul-Malik bin Abi Mahdhuurah si mtu maarufu, na Harith bin Ubayda pia kwake kuna maneno.[17]

3. Muhammad bin Is'hak bin Yasar bin Khiyar anasema: Kuwa masunni hawazitolei hoja riwaya zake. Amesema Ahmad bin Khushayma: Aliulizwa Yahya bin Mu'in juu yake huyo. Akasema: "Ni dhaifu kwangu, ni mgonjwa na hana nguvu."
Akasema Abul Hasan Al-Maymuni: "Nimemsikia Yahya bin Mu'in akisema, Muhammad bin Is'hak ni dhaifu. Na Nasaai amesema: "Yeye si mwenye nguvu."

4. Imekuja katika *Sunnan Ad-Darami*: "Hadith hii isnad yake ni dhaifu kwa sababu ya kuwepo Hafs bin Umar na baba yake, na Malik ametaja kisa hiki katika kitabu chake, *Muwattaa* kwa isnad yake yenye kukatika katika, ndani ya kitabu cha Swala.[18]

5. Muslim Bin Khalid bin Qurrah, ambaye huitwa Jarha alimtaja kuwa ni dhaifu Yahya bin Mu'in. Na akasema Ali Al-Madini: "Si chochote." Akasema Bukhari: "Hadith ni munkar." Nasaai naye amese-

14 *Tahdhiibul-Kamal* cha Jamalud-Din Al-Mazzi, Juz. 16, uk. 515 Na. 3755

15 *Tahdhiibul-Kamal* cha Jamalud-Din Al-Mazzi, Juz. 25, uk. 139 Na.178

16 *Mizanul Itidaalid-Dhahabi*, Juz. 3, uk. 631, Hadith Na. 7888

17 *Naylul Awtwaari*, cha Shawkani, Juz. 2, uk. 38

18 *Sunnan Darami*; Juz. 1, uk. 289

ma, mtu huyo hana nguvu katika upokezi." Naye Abul Hatim akasema kuwa mtu huyo hana nguvu katika upokezi na Hadith yake huandikwa lakini haitolewi hoja, hadith zake zajulikana na zapingwa."[19]

6. Tabrani amepokea katika kitabu *Al-Kabir* na pia Abdul Rahman bin Ammar bin Saad ambaye alisema kuwa Ibn Mu'in ni dhaifu katika Hadith.[20]

7. Na pia Abdul Rahman bin Qasit wala sikupata utajo wake.[21]

8. Tabrani amepokea katika Al-Awsat, akasema: "Mtu mmoja tu alijitenga kwake naye ni Marwan bin Thawban, nikasema, wala sikuona akitajwa mahali."[22]

9. Tabrani amepokea katika *Al-Awsat* na Saalih Al-Akhdhar, na wakakhitilafiana juu ya kumtolea hoja, na hakuna hata mmoja aliyemnasibisha ila kwa uongo tu.[23]

10. Amesema: "Na katika mlango, imepokewa kutoka kwa Abi Mahdhurah, amesema Abu Isa: "Hadith ya Bilal hatuijui ila Hadith ya Abu Israil Al-Malai. Na Abu Israil hakuisikia Hadith hii kutoka kwa Hakam bin Utaybah, akasema: "Yeye ameipokea kutoka kwa Hasan bin Umaarah kutoka kwa Hakam bin Utaybah, na Abu Israil jina lake hasa ni Ismail bin Is'haqa, huyu si mwenye nguvu miongoni mwa watu wa Hadith."[24]

---

19 *Tahdhiibul Kamal* cha Jamalud-Din Al-Mazzi; Juz. 37, uk. 508 Na. 5925

20 *Majmauz-Zawa'id*; Juz. 1, uk. 33

21 *Majmauz-Zawa'id*; Juz. 1, uk. 33

22 *Majmauz-Zawa'id*; Juz. 1, uk. 33

23 *Majmauz-Zawa'id*; Juz. 1, uk. 33

24 *Sunnan Tirmidhi*; Juz. 1, uk. 376 Na. 198

11. Riwaya hii ni dhaifu kwa sababu mwisho wake ni kutojulikana kutokana na neno lililomo ndani ya Hadith hiyo, 'watu miongoni mwa Answari.' Miongoni mwao ni Abu Umayr bin Anas. Ibn Hajar amemtaja na akasema juu yake kuwa amepokea miongoni mwa watu ma-Answari katika maswahaba wa Mtume (s.a.w.) juu ya kuona adhana ndotoni. Akasema Ibn Saad: "Alikuwa muaminifu lakini mwenye Hadith chache." Akasema Ibn Abdul Barri: "Hajulikani, hachukuliwi kwa kutolewa hoja."[25] Akasema Jamalud-Din: "Hii ndio iliyotokea kwenye maudhui mbili, kuona mwezi na adhana."[26]

12. Na katika riwaya hii:

a) Muhammad bin Ibrahim bin Al-Harith bin Khalid At-Tiimi Abu Abdallah, aliyefariki mwaka 120 (A.H.).

Amesema Abu Jafar Al-Aqiily: Kutoka kwa Abdallah bin Ahmad bin Hambali, nimemsikia baba yangu – akamtaja Muhammad bin Ibrahim At-Taymy Al-Madany, akasema: "Katika Hadith yake kuna kitu.. kwani yeye hupokea Hadith zinazokataliwa."[27]

b) Muhammad bin Is'hak bin Yasar bin Khiyar: Masunni hawazitolei hoja riwaya zake japokuwa yeye ndiye msingi wa *Sirah* ya Ibn Hisham.

Amesema Ahmad bin Abi Khaythama: "Aliulizwa Yahya bin Mu'in kuhusu mpokezi huyu, akasema: "Huyu ni dhaifu kwangu, hana nguvu."

25 *Tahdhibut-Tahdhiib* cha Ibn Hajar Juz. 12, uk. 188 Na. 867

26 *Tahdhibul Kamal* cha Jamalud-Din Al Mazzi Juz. 34, uk. 142 Na. 7545

27 *Tahdhibul Kamal* cha Jamalud-Din Al Mazzi Juz. 24, uk 304

Na akasema Abul-Hasan Al-Maymuni: "Nilimsikia Ibn Mu'in akisema:" Muhammad bin Is'hak ni mpokezi dhaifu. Na Nasai amesema: "Hana nguvu."[28]

c) Abdallah bin Zaid: "Inatosha kuwa yeye ana Hadith chache." Amesema Tirmidhi: "Hatujui Hadith yoyote kutoka kwake inayoswihi kutoka kwa Mtume (s.a.w.) ila Hadith ya adhana."

Amesema Hakim: "Ni sahihi kuwa yeye aliuwawa Uhud na riwaya zake zote zimekatika.

Amesema Ibn Adiy: "Hatujui Hadith yoyote kwake itokayo kwa Mtume (s.a.w.) ila ya adhana tu."[29]

Amepokea Tirmidhi, kutoka kwa Bukhari amesema: "Hatujui Hadith yoyote itokayo kwake ila ya adhana tu.[30]

Na Al-Hakim amesema: "Abdallah bin Zaid ndiye aliyeoteshwa adhana ambayo mafakihi wa kiislamu wamepokezana kwa kuikubali, lakini haikutoka kwenye *Sahih Muslim* na *Sahih Bukhari* kutokana na kuhitilafiana wenye kuipokea katika sanad zake.[31]

13. Sanad ndani yake muna: Muhammad bin Is'hak bin Yasar na Muhammad bin Ibrahim At-Taymi na umekwishajua hali zao kama vile ulivyojua kuwa Abdallah bin Zaid ambaye alikuwa amepokea riwaya chache tu, na zote zimekatika.

---

28 *Tahdhibul Kamal* cha Jamalud-Din Al Mazzi Juz. 24, uk. 423 na angalia *Tarikh Baghdad*; Juz. 1, uk. 221- 224

29 *Sunnanut-Tirmidhi*; Juz. 1, uk. 361. *Tahdhibut-Tahdhib*: Ibn Hajar Juz. 5 uk. 224

30 *Tahdhibul Kamal* cha Jamalud-Din Al-Mazzi Juz. 14, uk. 541

31 *Mustadrak* cha Hakim Juz. 3, uk. 336

14. Katika sanad za riwaya hii ameingia Muhammad bin Is'hak bin Yasar na Muhammad bin Al-Harith At-Taymi na Abdallah bin Zaid, na makosa ya wawili hao wa mwanzo umeyatambua na kule kukatika sanad za kila walichopokea kutoka kwa watatu, kwa hivyo hapa ile hali ya sanad yaonekana wazi, angalia kwa makini.

Njia ya pili: Namna riwaya hizo zilivyotaja namna ya kuwekwa adhana kunaenda kinyume na misingi maarufu ya kuwekwa hukmu

Katika sehemu hii ya utafiti tutaonyesha namna riwaya hizo zinavyokwenda kinyume na njisi ya kuwekwa adhana kwa nukta zifuatazo:

Kwanza haziwafikiani na daraja ya utume, kwani Mwenyezi Mungu (S.W.T.) amemtuma Mtume (s.a.w.) kwa kusimamisha Swala na waumini katika nyakati tofauti, na bila shaka ilivyo atamfundisha namna ya kutimiza hilo, kwa hivyo haina maana Mtume (s.a.w.) awe kwenye kukanganywa kwa siku nyingi au siku ishirini au kama katika riwaya aliyoipokea Abu Daud akiwa Mtume (s.a.w.) hajui jinsi atakavyohakikisha majukumu yaliyoko shingoni kwake, mara awe amuomba huyu na mara yule, ndipo apate kufikia lengo lake na ilhali Mwenyezi Mungu (S.W.T.) amesema: "Fadhila za Mwenyezi Mungu kwako zimekuwa ni kubwa."[32] Na makusudio ya fadhila hapa ni elimu, kwa kulinganisha na Aya iliyo kabla ya hiyo isemayo: "na akakufundisha uliyokuwa huyajui.."

> Swala na Saumu ni katika mambo ya kiibada, na si kama vita ambapo Mtume (s.a.w.) saa nyingi akiwashauri swahaba wake, na ushauri wake haukuwa juu ya jinsi ya kupigana kwa sababu eti alikuwa hajui lililo na maslaha zaidi bali kwa ajili ya kuzivuta

32 ***Nisaa : 113***

nyoyo zao kama anavyosema Allah: **"Na lau ungekuwa ni mkali, mgumu wa moyo basi wangelikukimbia walio pembeni (karibu) nawe. Basi wasamehe, waombee msamaha na uwashauri katika mambo na ukiazimia (kufanya jambo), mtegemee Mwenyezi Mungu...[33]"**

Je huku si kuitweza dini? Iwe ndoto tu zilizootwa na watu wa kawaida iwe ndio msingi wa mambo ya kiibada na la muhimu kama la adhana na iqama? Hii inatufanya tuseme kuwa jambo la kuwa ndoto ndio inayoweka sheria twasema kuwa ni jambo la uongo la kumzulia Mtume (s.a.w.) na hapana shaka watu wa Abdallah bin Zaid ndio walioeneza jambo hilo la ndoto ili iwe fadhila katika nyumba yao na kabila yao, kama ilivyo katika riwaya ya kwamba kumi na wawili katika watu wake ndio wapokezi wa Hadith hii na aliowategemea ilikuwa ni kwa ajili ya dhana nzuri kwao tu.

Pili: Riwaya hizo juu ya adhana zinapingana kwa pande hizi: Muktadha wa riwaya ya kumi na mbili – Riwaya ya Abu Daud ni kwamba Umar bin Al-Khatab aliota adhana kabla ya Abdallah bin Zaid kwa siku ishirini, lakini riwaya ya kumi na tatu – ya Abu Daud - yeye aliota usiku ule ule alioota Abdallah bin Zaid.

Kwamba ndoto ya Abdallah bin Zaid ndio chanzo cha kuwekwa adhana na si ya Umar bin Al-Khattab kwani Umar alisikia adhana baada ya hapo akaja kwa Mtume (s.a.w.) na akasema kwamba yeye pia aliota ndoto kama hiyo lakini hakuitaja kwa kuona haya."

Aliyeanzisha hasa ni Umar bin Al-Khattab mwenyewe na si ndoto yake kwani yeye ndiye aliyependekeza mwito wa Swala ambayo

[33] ***Aali-Imran: 159***

ndiyo adhana. Tirmidhi amepokea katika *Sunnan* yake kuwa amesema: "Walikuwa waislamu wanapokuja Madina….mpaka aliposema, wakasema baadhi yao pigeni parapanda kama parapanda la mayahudi. Akasema: "Akasema Umar bin Khattab: "Kwanza si mtafute mtu atakayenadi kuwaita kwenye Swala?" Akasema: Akasema Mtume (s.a.w.) Ewe Bilal Simama na unadi kwa ajili ya Swala."

Ibn Hajar ameieleza kuwa mwito wa Swala makusudio yake ni ile kusema: الصلاة الجَمِي "*Swalaatu jamia'*[34] Wala hakuna dalili ya maelezo haya yake. Bali iko karibu na maelezo yenu, yaani ya adhana inayotegemewa.

Kisha msingi wa kuwekwa adhana ni Mtume (s.a.w.) mwenyewe. Amepokea Bayhaqi: "Wakataja kuwa wapige parapanda au wawashe vijinga vya moto akaamrishwa Bilal me aadhini na kuifuatiza na iqama. Amesema: "Amepokea Bukhari, kutoka kwa Muhammad bin Abdul Wahab. Na amepokea Muslim kutoka kwa Is'hak bin Ammar.[35] Pamoja na hitilafu hizi nyingi katika kunakili Hadith vipi itawezekana kuitegemea?

Tatu: Walioota ni watu kumi na wane na si mmoja pekee

> Inadhihiri kwa aliyopokea Al-Halabi kwamba aliyeota adhana si Ibn Zaiyd na Umar peke yao bali pia alidai Abdallah Abu Bakr. Imesemekana pia ma-Answari saba waliota adhana. Ikasemekana pia kumi na wane.[36]

34 *Fat'hul-Bari* cha Ibn Hajar Juz. 2, uk. 81. Chapa ya Darul-Maarifah

35 *Sunnan Al-Bayhaqi*

36 *Sirah* ya Ibn Halabiyyah; Juz. 2, uk. 95 Chapa ya Daru turathi arabi

Wote hao wamedai waliona adhana ndotoni. Ikiwa sharia na hukmu zafuata ndoto basi Uislamu uhifadhike!! Ambapo Mtume (s.a.w.) hupokea sharia kutokana na wahyi na si ndoto.

Nne: Kuna mgongano kati ya riwaya ya Bukhari na zingine

Bukhari aeleza kuwa Mtume (s.a.w.) alimwamuru Bilal katika baraza la mashauriano kuwa aadhini, na Umar alikuwapo wakati wa amri hiyo.

Imepokewa kutoka kwa Ibn Umar: "Walikuwa waislamu wanapokwenda Madina wakikusanyika na kuswali kukiwa hakuna mwito wa kuwaita, siku moja wakalizungumzia jambo hilo. Wengine wakasema, pigeni kengele kama manaswara. Bali wengine wakasema, pigeni parapanda kama mayahudi, Umar akasema: "Je hamumtumi mtu akanadi kwa Swala? Hapo Mtume (s.a.w.) akasema: "Simama ewe Bilal unadi Swala."[37]

Na ilivyo wazi ni kuwa Mtume (s.a.w.) alimuamuru Bilal kuadhini wakati wa Swala ya Alfajiri. Kwani alihadithiwa na Abdallah bin Zaid juu ya ndoto yake na Umar hakuwapo, yeye aliisikia adhana akiwa nyumbani kwake akatoka huku akikokota nguo yake na akisema: "Naapa kwa aliyekutuma kwa haki ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.), hakika nimeota kama alivyoota yeye."

Hatuwezi kuchukua aliyopokea Bukhari juu ya kusema الصلاة الْجَمِي *'swalaatu jaamia'* na kuchukulia riwaya zisemazo juu ya kuadhini kwa adhana kwani, kwanza zimekusanywa bila ya ushahidi, lau Mtume (s.a.w.) angelimuamuru Bilal kuinua sauti katika kusema "*swalaatu jaamia*" basi kifungu cha kwanza kingelikuwa halali na

37 *Sahih Bukhari*; Juz. 1, uk. 301 Mlango wa Adhana. Chapa ya Darul qalam, Lebanon

kungeliondoka shaka hasa katika kukariri jumla ya 'swalaatu jaamia' na kusingekuwa na wasiwasi, hii ni dalili kuwa amri ya mwito ilikuwa ya kuadhini kwa adhana hii iliyowekwa.[38]

Njia ya tatu: Hukmu ya – As-Swalatu khayrun minan nawmi - kuongezea katika adhana kwa wanavyuoni wote

Amesema Shafi'i: "Sipendi kuongeza maneno katika adhana ya Swala ya alfajiri wala katika nyingine, kwa sababu Abu Mahdhur hakupokea kutoka kwa Mtume (s.a.w.) yeye aliamuru kuongeza nami nachukia kuongeza katika adhana na kuongeza kitu baada ya adhana,"[39]

Na amesema mwenye kitabu cha *Bidayatul-Mujtahid*: "Wamehitilafiana katika kauli ya muadhini katika Swala ya Alfajiri ya **الصلاة خير من النوم** *As-swalaatu khayrun minan nawm*' je husemwa au la? Wengi wakasema kuwa husemwa, wengine wakasema kuwa haisemwi kwa sababu neno hilo halimo katika adhana ya Sunna na Shafi'i pia amesema hivyo. Na sababu ya hitilafu yao ni je hilo lilisemwa wakati wa Mtume (s.a.w.) au wakati wa Umar?

Qurtubi naye amesema katika Tafsiri yake: "Wamekhitilafiana katika kuongeza neno ' **الصلاة خير من النوم** *Aswalaat khayrun minan nawm*' hiyo ni kauli ya Shafi'i Iraq na Misri alisema kuwa hasemi hivyo.[40]

Amesema Hasan bin Hasan: "Neno hili hatulisemi pia kwa sababu halikuja kutoka kwa Mtume (s.a.w.)." [41]

---

38 *An-Nass wal-Ijtihad* cha Sharafud-Din; uk. 200

39 *Al-Ummu*; Juz. 1, uk. 104. Chapa ya Darul fikri, Beirut mwaka 1403 (A.H.)

40 *Tafsir Qurtubi* Juz. 6, uk. 228 Chapa ya Daru Ihyaai turath, 1405 (A.H.)

41 *Al-Muhalla;* Juz. 3, uk. 161 Chapa ya Daru Ihyaai turath, Beirut

Na imepokewa kutoka kwa Abu Hanifa kama ilivyo katika *Jamiul-Masanid,* kutoka kwa Hammad bin Ibrahim amesema: "Nilimuuliza juu ya kuongeza neno: *as-swalatu khayrun minan nawmi?* akasema kuwa hivyo ndivyo walivyozusha watu, nayo ni mazuri katika waliyozusha."

Na wametaja kuwa (*as-swalatu khayrun minan nawmi*) ilikuwa baada ya muadhini kumaliza adhana yake – kuwa - (as-swalaatu khayrun minan nawmi) mara mbili.

Alisema: Ameitoa - Imam Muhammad bin Hasan Ash-Shaybani kutoka kwenye, athari, wakaipokea kutoka kwa Abu Hanifa. Kisha akasema Muhammad: "Nayo ni kauli ya Abu Hanifa na tunachukua kutoka kwake."**42**

Shafi'i katika kauli yake ya zamani alisema: *as-Swalaatu khayrun minan nawmi* ni sheria, na kauli mpya akasema ni makruh nayo ilipokewa kutoka kwa Abu Hanifa, lakini walihitalfiana na katika mahali pake kauli iliyo mashuhuri ni kuwa katika Swala ya Alfajiri tu.

Na kutoka kwa An-Nakhaii na Abu Yusuf kwamba hiyo ni Sunna katika kila Swala.

Na amepokea Ash-Shaabi na wengineo kwamba imesuniwa kuwa katika Swala za Isha na Alfajiri.

Itra - yaani Ahlul-bayt – na Shafi'i katika moja ya kauli zake mbili amesema kuwa – as-Swalaatu khayru minan nawmi ni bidaa.

Amesema katika *Al-Bahri* kuwa ameizusha Umar. Mwanawe akasema: "Hii ni bidaa. Na kutoka kwa Ali , alipoisikia alisema: "Msiongeze kitu kisicho ndani ya adhana." Kisha akasema baada ya

42 *Jaamiul Masanid* cha Khawarzami Juz. 1, uk. 296

kutaja Hadith ya Abu Mahdhurah na Bilal.

Tunasema: Lau ingekuwa baada ya kuikanusha Ali Ibn Umar na Taus, tumekubali hivyo basi amri yetu ni kujulisha hali ilvyokuwa – sio kufanya sheria, hivyo ni kukusanya kati ya Aathaar."[43]

Amesema Nawawi: "Ama kuongeza maneno katika Swala ya Alfajiri hapo kuna njia mbili, ya sahihi ni ile aliyoiamua mtunzi na wanavyuoni wengine kwamba ni Sunna kwa Hadith ya Abu Mahdhurah. Na njia ya pili kuna kauli mbili, mojawapo ni hii ya zamani ameinakili Kadhi na Abu Tayyib na mwenye kitabu *Shamil* kutoka kwa nassi ya Shafi'i katika *Al-Buwayti* kwa hiyo ambayo inakuwa imetajwa katika kauli ya zamani na mpya, na ameinukuu mwenye kitabu *Tatimmmah* kutoka nassi ya Shafi'i ndani ya vitabu vyake vyote.

Pili: Nayo ni kauli mpya, kwamba ni makruh na aliyekata kwa njia yake kauli mbili Darmi, na imam wa haram mbili akadai kuwa hiyo ni mashuhuri zaidi. Na kwa madhehebu ni kwamba hiyo imewekwa, kwa hiyo, hiyo ni Sunna hata kama itaachwa basi adhana itaswihi bali itakosekana fadhla tu, na hivi ndivyo walivyoamua wenzake.[44]

Amesema Amir Al-Yamani As-Sanaani katika kitabu chake '*Subulus-Salaam'*: "Nimesema neno hilo la *'Swalatu khayrun minan nawm*' si katika maneno ya adhana iliyowekwa kwa ajili ya kunadi Swala na kuwapa watu habari kwamba Swala imeingia wakati wake, bali ni maneno yaliyowekwa kumuamsha aliyelala nayo ni kama matamshi ya tasbihi waliyozowea watu kuyasoma katika hizi zama za mwisho mwisho, ukilijua hili basi itakuwia rahisi mazoea ya wanavyuoni ya mjadala juu ya kuongeza maneno hayo. Kuwa je ni katika maneno ya

43 *Naylul Awtwaar* cha Shawkani Juz. 2, uk. 28 Chapa ya Darul Kutub, Beiru

44 *Al-Majmuu* cha Nawawi Juz. 3, uk. 92

adhana au la? Na je ni bida'a au la?

Kisha makusudio yake ni kuamsha kwa ajili ya Swala kwamba Swala ni bora kuliko usingizi."[45]

Amesema Nawawi katika ufafanuzi wake kwenye kitabu '*Sahih Muslim*': "Jua ya kwamba ni Sunna kumjibu muadhini kwa kauli kama aisemayo kwa kila anayemsikia kwa aliye tahara au aliye na najisi, au aliye na janaba au hedhi na wengineo ambao hapana kizuizi kwa kujibu, sababu za kuzuia kujibu ni kama vile mtu kuwa chooni au kuwa katika tendo la ndoa au mfano wa mawili hayo, pia kwenye Swala, anayekuwa katika Swala ya faradhi au ya Sunna na akasikia adhana hatofaa kuijibu hapo, ama akimaliza Swala atajibu. Na lau atafanya hivyo akiwa ndani ya Swala, je ni makruhu?

Hapo kuna kauli mbili, za Imam Shafi'i, iliyodhihiri sana ni ile ya kuwa ni makruhu kwa sababu ni kuingilia Swala, lakini haibatilishi Swala yake. Akisema tuliyoyataja kwa sababu ni tajo. Lau atasema, **حَي على الصلاة** 'Hayya ala Swalaa' au **الصلاة خير من النوم** As-swalaatu khayrun minan nawm' basi Swala yake itabatilika akiwa anajua uharamu wake kwa sababu hayo ni maneno ya kibinadamu."[46]

Njia ya nne: Kusema الصلاة خير من النوم Aswalaatu khayrun minan nawm ni katika ijtihadi ya Khalifa wa nne

Ikiwa haikuthibitishwa usahihi wa riwaya zinazoonesha adhana ilivyokuwa kuligana na sanad na dalili zake, basi hapana nafasi ila kuamini kuwa usahihi wa riwaya zinazonakili kuongeza '*as-Swalaatu*

45 *Subulus-Salaam*; Juz. 1, uk. 167 Chapa ya Daru Ihyaai turath, Beirut.

46 Sherhe ya *Sahih Muslim* Jz. 2, uk. 88 Chapa ya Darul kitabil arabi, Beirut 1407 (AH.)

khayrun minan nawm' katika adhana ilikuwa ni ijtihad ya khalifa wa pili Umar bin Khattab na kwamba haikuwekwa wakati wa Mtume (s.a.w.), hebu angalia riwaya zinazotaja hilo:
Imepokewa kutoka kwa Malik kwamba ilimfikia ya kuwa muadhini alikwenda kwa Umar bin Khatab ili aadhini kwa Swala ya Alfajiri, akamkuta amelala, akasema: "Aswalaatu khayrun mina nawm" Umar akamwamrisha aiweke kwenye adhana ya Alfajiri.

Amesema Zarqani: "Hii ameitoa Daru Qutni katika *Sunnan* kutoka kwa njia ya Wakii katika utungo wake, kutoka kwa Al-Amri, kutoka kwa Nafii, kutoka kwa Ibn Umar kutoka kwa Umar, na ameitoa pia kutoka kwa Sufyan, kutoka kwa Muhammad bin Ajlan, bin Nafii, kutoka kwa Ibn Umar, kutoka kwa Umar amesema: "Alimwambia muadhini wake ukifika mahali pa kusema "*hay'ya alaal falah*" katika Swala ya Alfajiri, sema '*As-Swalaatu khayrun minan nawm* (mara mbili) **الصلاة خير من النوم** Ibn Abdu Rabbi akapunguza katika maneno yake akisema: "Sijui hii iliopokewa kutoka kwa Umar kwenye njia isiyotolewa hoja na isiyojulikana usahihi wake!"**47**

Imepokewa kutoka kwa Jarih, amesema amenipa habari Hasan bin Muslim ya kwamba mtu mmoja alimuuliza Taus ni wakati gani ilisemwa 'Aswalaatu khayrun minan nawm.' Akasema: "Ama haikusemwa wakati wa Mtume (s.a.w.), lakini Bilal aliisikia enzi za Abu Bakr baada ya kufariki Mtume (s.a.w.) akiisema mtu ambaye hakuwa muadhini akaichukua kutokwa kwake. Akaadhini na kuitaja. Abu Bakr alikaa kidogo mpaka akaja Umar akasema: "Lau tunge-limzuia Bilal na haya kama aliyesahau, kwa hivyo akawaambia watu wataje kwenye adhana mpaka leo."**48**

47 *Sharhe Zarqani* Juz. 1, uk. 194, na Sherhe ya Zarqani ya *Muawata* ya Imam Malik Juz. 1, uk. 243

48 *Kanzul-Ummaal;* Juz. 8, uk. 357 na *Musannif Abdu Razaq Sanaani* Juz. 1, uk. 474

Imepokewa kutoka kwa Ibn Jarih amesema: "Ameniambia Umar bin Hafs kwamba Saad ndiye aliyeanza kusema 'Aswalaatu khayrun minan nawm' katika ukhalifa wa Umar, akasema hiyo ni bida'a kisha akaiacha, na kwamba Bilal hakuadhini tena." kwa ajili ya Umar.

Njia ya tano: Maoni ya wanavyuoni wa Shi'a juu ya kuongeza maneno kwenye adhana

Sayyid Murtadha amesema: "Kuongeza maneno – as-Swalaatu khayrun minan nawmi - katika adhana ya Swala ya Alfajiri ni bida'a, hii ni sahih na ndivyo wanavyosema watu wetu. Wamekhitilafiana mafakihi je *tathwibu* ni nini?

Shafi'i akasema: "*Tathwibu* ni kusema baada ya mwito wa Swala 'Aswalaatu khayrun minan nawm' mara mbili."

Na imepokewa kutoka kwa Abu Hanifa kuwa amesema: "*Tathwibu* ni kusema baada ya kumaliza adhana '*Hay'ya a'la swalaa' hay'ya a'lal falaah*' mara mbili.

Na imepokewa kutoka kwa Muhammad, amesema katika vitabu vyake: "Mwanzo Tathwibu ilikuwa ni kusema 'Aswalaat khayrun minan nawm' kati ya adhana na iqama. Kisha watu wa mji wa Kufa wakayazua maneno, *'Hay'ya a'la swalaa, hay'ya alal falaah'* mara mbili baina ya adhana na iqama.

Shafi'i naye amesema kuwa kuongeza ni Sunna katika Swala ya Alfajiri pekee na si zingine.

Na imepokewa kuwa yeye alisema katika kauli mpya kuwa "Si Sunna."

An-Nukhai naye amesema: "Ni Sunna pia katika Swala zingine."

Dalili ya kuswihi tusemavyo ni kuwa lau kuongeza kungelikuwa kumewekwa kisharia basi ingepasa kuwe na dalili ya kisharia kabisa lakini hakuna. Aidha hakuna ikhtilafu kuwa mtu akiacha kuongeza maneno hayo hatolaumiwa kwa sababu ama itakuwa kauli hiyo ni Sunna kulingana na kauli za baadhi ya mafakihi, au si Sunna pia kulingana na mafakihi wengine. Kwa hiyo katika kila moja ya mawiili hayo hakuna atakayelaumiwa kwa kuacha, na ikiwa hakuna makosa katika kuacha na kuogopa kuwa kufanya hivyo ni bida'a na maasi, basi kuacha ni bora zaidi na ni kujitoa shaka katika sharia,"[49]

Sheikh Tusi amesema: "Sio Sunna kuongeza katika hali ya kuadhini hata baada ya kumaliza kuadhini, nayo ni ile mtu asemaye: useme '*As-swalaatu khayrun mnan nawm*' katika Swala zote. Dalili ya kukataa kwetu iko mahali pawili, kwamba kuithibitisha kuwa yafaa wakati wa adhana na kati ya adhana na iqama kunahitaji dalili, na katika sharia hakuna linalothibitisha"[50]

Allama Hilli amesema: "Tathwibu kwetu sisi ni bida'a (yaani kusema Aswalaatu khayrun minan nawm'). Mpaka akasema: Na haya yote kwetu ni batili, kwa sababu Nabii (s.a.w.w) haimfalii afanye ijitahidi katika hukmu, bali yeye huzichukua kwa wahyi si kwa njia ya istihsani (**Istihsani**: **Ni kutoa mapendekezo kisha hutizamwa, hili ni zuri liwekeni katika sharia).**

Kisha alisema: Pia katika Swala ya Alfajiri hakuna kuongeza maneno tathwibu kwetu, na pia katika nyingine. Na pia wanavyuoni wengi hawataki nyongeza hiyo, kwa sababu Ibn Umar siku moja aliingia

49 *Masa'ilun Nasiriyyat*; uk. 181 – 182 Chapa ya Rabitatu thaqafa, Tehran.

50 *Al-Khilaaf*, Juz. 1, uk. 286-287 Chapa ya Jamaatul Mudarrisiina, Qum.

msikitini akamsikia mtu akifanya Tathwibu, katika adhana ya Adhuhuri, basi akatoka, alipoulizwa kwa nini alitoka, alijibu: "Nimetolewa na bida'a."

Na imepokewa kutoka kwa Hasan bin Swaleh bin Hayyi kwamba yeye aliipendelea katika Swala ya Isha kwa sababu ni wakati watu wanapolala."

Nukhai naye amesema: "Ni Sunna katika Swala zote, kwa sababu kinachokuwa Sunna katika Swala moja basi chafaa katika Swala zote."**51**

Sheikh Mawla Ahmad Ardabili amesema katika kitabu chake '*Majmaul faaida wal'burhan:* "Ama kuwa kusema 'Aswalatu khayrun minan nawm ni bida'a ni kwa sababu hilo halikunukuliwa, bali katika hadith pia hakulijua (s.a.w) ilipokewa kwa Hasan (Ibrahim) juu ya kuongeza maneno je ni vipi? Akasema: "hatulijui hilo - yaani hatulisemi hilo"**52** …La msingi huko ni kufanya sharia, na kuibadilisha Adhana ilionakiliwa na ni ziyada iliyo badala ya ile iliyothibiti kisheria, hivyo basi inakuwa haramu. 52

Imepokewa kutoka kwa Muawiya bin Wahab amesema: "Nilimuuliza Abu Abdallah juu ya kuongeza maneno katika adhana na iqama, aka-jibu: "Hatulijui hilo."

Amesema Majlisi: "Hatulijui hilo." Yaani halikuwekwa kisharia. Kwani lau lingeliwekwa kisharia basi tungelilijua."

---

51 *Tadhkiratul Fuqaha'a*; Juz. 3, uk. 49-50

52 *Majmaul Fa'ida,* Juz. 2, uk 177-178

Na amesema katika *Al-Muntaha*: "Kuongeza neno la aswalaatu khayrun minan nawm' katika adhana ya Swala ya asubuhi na nyingine si jambo lililowekwa kisharia kama walivyosema wanavyuoni wetu wengi na pia Shafi'i amesema hivyo hivyo. Na masunni wengi pia wamelipendelea liwe wamelifanya kuwa sunna katika Swala ya Alfajiri.

Lakini kutoka kwa Abu Hanifa kuna riwaya mbili katika namna ya yake ya kwanza ni kama tulivyosema na nyingine, kwamba tathwib ni tamko la muadhini kati ya adhana ya Alfajiri na Iqama yake kusema ' Hayya a'las-Swalaa' (mara mbili na hayya a'lal falaah (mara mbili). Amesema katika *An-Nihaya*: "Ndani yake itakapofuatiwa na Swala basi ileteni kwa utulivu na tathwibi hapa ni kukimu kwa Swala, na asili ya tathwibi ni kuwa mtu aje huku akipiga kelele akiomba na kudhihirisha nguo yake ili aonekane, ndipo dua ikaitwa *tathwib* kwa ajili hiyo.

Imesemwa pia katika lugha ya kiarabu neno, *thaaba, yathuubu* mtu anaporejea, hivyo ni kurejea kwenye jambo kwa haraka katika kufanya haraka kwa Swala. Muadhini asemapo: "*Hayya a'la swalaa"*, basi huwa amewaita watu kwenye Swala; na akisema baada ya neno hilo: "As swalaatu khayrun minan nawm" huwa amerudia kwenye neno hilo, kwa hiyo maana yake ni kufanya haraka kwenda kwenye Swala.

Amesema katika *'Hablul matin*: "baada ya kuotoa riwaya kama hivi juu ya tathwib ambayo inakuwa baina ya adhana na iqama, hiyo yaonyesha kutowekwa tathwib baina ya adhana na iqama. Na wamekongamana ulama wetu kwa kuacha tathwib iwe imefafanuliwa kwa maana hii au kwa kauli ya, *Aswalaatu khayrun minan nawm*.[53]

53 *Mir'aatul u'quul,* Juz. 15, uk. 83 hadith 6

Amesema Sheikh Muhammad Hasan Najafi katika kitabu chake *'Jawaahirul-kalaam*: "Tahwibi katika adhana, kama ilivyo mashuhuri kati ya watu wa ilmu ya lugha na Fiqh, ni kutamka: "As swalaatu khayrun minan nawm' watu wetu wamekongamana, juu ya kutowekwa neno hilo, isipokuwa wachache miongoni mwao. Dhahiri ni kutokuwana tofauti kati ya tathwibi kuwa ni makruh au haram, kwa maana hii ni kati ya kuleta baada ya 'hayya a'lal falaah kama wafanyavyo Sunni na kuleta baada ya hayya a'laa khayril a'mal."[54]

Njia ya Sita: Namna ya kuwekwa adhana kwa madhehebu ya Ahul bayt

Tunapoangalia riwaya za Ahlu Bayt juu ya mwanzo wa kuwekwa adhana hatuoni kama tuliyoyaona hayo yaliyotangulia, nayo ni kwenda kunyume na daraja ya utume, miongoni mwazo ni:

1. Katika Wasaail kwa isnadi yake kutoka kwa Muhammad bin Ali Mahbuub, kutoka kwa Ali bin As-Sunni, kutokwa kwa Bin Abi Umar, kutoka kwa Ibn Udhayna, kutoka kwa Zurara na Alfadhail bin Yasar, kutoka kwa Jafar (a.s.) amesema: "Mtume (s.a.w.) alipopelekwa Israi, alipofika baytul maamuur ulifika wakati wa Swala, Jibril akaadhini na kisha akakimu, Mtume akatangulia kuswalisha, wakapiga safu malaika na mitume nyuma yake, Akasema: 'tukasema: Je aliadhini vipi? Akasema: "Alisema, Allahu Akbar, Allahu Akbar, ash-hadu anlaa ilaaha illa llah, ash-hadu anna Muhammadan rasuulu'llah, ash-hadu annau Muhammadan rasuulu llah hayya ala swalaa, hayya ala swalaa, hayya alal falaah, hayya alal falaah, hayya alaa khayril-amal, hayya alaa khayril amal, Allahu Akbar Allahu Akbar, laailaaha illa'l-lah, laailaaha illa'llah. Na iqama ni kama hiyo ila katika iqama kuna; 'Qad qaaamati swalaa, 'Qad qaaamati swalaa, baina ya hayya ala

54 *Mu'ujamu Fiqhil Jawaahir*, Juz. 1, uk. 207

khayril amal na baina ya allahu akbar. Mtume akamuamuru kufanya hivyo Bilal, na aliendelea kufanya hivyo mpaka Mtume alipoaga dunia."**55**

2. Imepokewa kutoka kwa Muhammad bin Ali bin Husein kwa isnad yake kutoka kwa Hafsa bin Al-Bakhtari, kutoka kwa Abi Abdillah (a.s.) amesema; 'Alipopelekwa Mtume (s.a.w.w.) israi na ukafika wakati wa Swala, Jibril aliadhini na kisha aliposema, Allahu Akbar Allahu Akbar, malaika nao wakasema, Allahu Akbar Allahu Akbar, aliposema ash-hadu anlaa ilaaha illa llah, malaika wakasema, "amewavua waliojifananisha na Mwenyezi Mungu." Aliposema, ash-hadu anna Muhammadan rasuul'llah, Malaika wakasema: "Ni mtume aliyetumwa." Aliposema, hayya ala swalaa' wakasema: "Amehimiza juu ya ibada ya Mola wake." Aliposema hayya alal falaah, wakasema: "Amefaulu mwenye kumfuata."**56**

Imepokewa kutoka kwa Abi Abdillah Sadiq (a.s.) amesema: "Jibril aliposhuka kwa Mtume kwa ajili ya adhana, Mtume (s.a.w.w.) alikuwa kwa Ali, Jibril akaadhini na akakimu, Mtume alipoamka, akasema: "Ewe Ali, je umesikia?" Akajibu, ndio akamwambia, je umeihifadhi? Akamjibu, ndio. Mtume akasema: "Mwite Bilal umfundishe." Ali akamwita Bilal na akamfundisha."**57**

Riwaya hizi zinatilia nguvu riwaya za Asqalani alizozitaja na kujadii katika isnadi zake. Akasema: Zimekuja Hadith zinazojulisha kwamba Adhana iliwekwa Makka kabla ya Hijra, kati ya hizo ni kwa Tabrani

55 *Al-Wasail*, Juz. 5. uk.146 hadith 6969. *Tahdhib*, Juz. 2, uk. 60 hadith 21, *Al-Istibswa*ar, juz. 1. uk 350, Hadith 1134 na katika *al-Kafi*, Juz. 2, uk. 20 hadith 2 mlango wa Adhan na Iqama

56 *Al- Wasaail* Juz 5 uk. 417 Hadith 6971

57 *Al- Wasaail* Juz 4 uk. 612 Milango ya adhan na iqama Hadith 2

kutoka kwenye njia ya Salim bin Abdallah bin Umar kutoka kwa baba yake, amesema: "Mtume alipopelekwa israi, Mwenyezi Mungu alimpa wahyi wa adhana, akateremshiwa wahyi huo na akamfundisha Bilal. Na katika isnad ya Talha bin Zaid nayo imeachwa.

Na Darqutni katika kitabu chake *'Al-Atraf'* kutoka kwa Hadith ya Anas: "Kwamba Jibril alimwamuru Mtume kuadhini ilipofaradhiwa Swala." Amesema: Isnad yake hii ni dhaif."

Na Ibn Murdawayh kutoka kwa Hadith ya Aisha, ni marfuu': 'Mtume asema, nilipopelekwa israi, Jibril aliadhini, na malaika wakadhani kwamba Jibril atawaswalisha, yeye akanitanguliza nikawaswalisha." Amesema: " katika hadith hii kuna yule tusiyemjua."

Na Bazar na wengine wana hadith ya Ali, amesema: "Mwenyezi Mungu alipotaka kumfunza adhana Mtume, Jibril alimpeleka tume mnyama aitwaye 'Buraq', akampanda. Akataja Hadith hiyo.**58** Katika isnad yake Ziyad bin Al Mundhir Abul Jaarud, nayo pia imeachwa. Inawezeka katika kukadiria kuwa sahihi ni kule kuchukuliwa kutajwa israi mara nyingi inakuwa hiyo imetokea Madina. Na ukweli ni kwamba hakuna usahihi wowote katika Hadith hii.

Riwaya hizi alizozinukulu Asqalani zinaonyesha wazi juu ya madhehebu ya Ahlu-bayt katika kuwekwa adhana.

Ama mjadala wa Asqalani katika sanad zake alikuwa aithibitisha kuwa mwanzo wa kuwekwa adhana ni ndoto ya Abdallah bin Zubeir au Umar bin Al-Khattab, kubatilika kwa maombi hayo kumetajwa hapo mbeleni. Na anayetaka kupata uhakika wa uwanja huu na aangalie mambo yafuatayo:

58 *Fat'hul-Bari fi Sharhil-Bukhari*, juz. 2, uk. 89 Chapa ya Darul maarifa, Lebanon

Marejeo ya pande mbili kwa wingi kwamba nassi zinazosisitiza juu ya mwanzo wa adhana na iqama ni amri ya Mtume (s.a.w.) alipomuamuru Bilal, hebu chukua mfano:
1. Hadith iliyotajwa na Bukhari kutoka kwa Anas bin Malik amesema: "Watu walipozidi kutaja juu ya kuwepo alama ya kuwajulisha Swala, wakataja kuwashwe moto au wapige parapanda, ndipo akamuamuru Bilal aadhini na akimu."**59**

Hebu angalia kwa ufafanuzi wapokezi wa Hadith hii:
a) Umar bin Maysara Al-Manqari:
Daru Qutni na Ibn Hajar wamesema kuwa huyu ni mkweli.

b) Abdul Warith bin Said Abu Ubayda Al-Anbari Al-Basri At-Tannuri: Nasaba yake katika kitabu *Tahdhib* ni Ibn Sa'id ibn Dhakwan at-Tanauri, yeye ni mmoja katika wanachuo mashuhuri. Abu Zar'a amesema: "Mtu huyu ni mkweli."

Na Abu Hatim akasema: "Ni mkweli."**60**

c) Khalid Al-Hadhaa amesema: "Amesema Ahmad ni mtu thabiti: Amesema Ibn Mu'in: 'Mtu huyu ni mkweli." Hata Nasai pia amesema hivyo.

Abu Hatim amesema: "Huyo Hadith zake zimeandikwa lakini hazitolewi hoja." Fahd bin Habban akasema: "Alikuwa na haiba na alikuwa na Hadith nyingi."**61**

d) Abu Qalabah Al-Jarmiy Abdallah bin Zaid bin Umar Al-Basri: Amemtaja Ibn Sa'ad katika kitabu chake *Tabaqat* ya pili kutoka katika watu wa Basra, na alikuwa na Hadith nyingi."**62**

59 *Fat-hul Bari fi Sharhil Bukhari*; Juz. 2, uk. 77 Mlango wa mwanzo wa adhana

60 *Rijal Sahihul Bukhari*: *Al-Kalabadhi*, Juz. 2 Uk. 574

61 *Rijal sahihul Bukhari: Al-Kalabadhi*, Juz. 1 Uk. 227

62 *Thahibut-Tahdhiib*, Juz. 5, uk. 224

e) Anas bin Malik bin Nadhr, mtumishi wa Mtume (s.a.w.) ni mgeni wa Basra.

Amesema Bukhari katika *Tarikhul-Kabir*, kutoka kwa Qatada: "Alipokufa Anas bin Malik, Muwarriq alisema, "Leo imeondoka nusu ya ilimu." Akaulizwa: "Vipi?" Akajibu: "Huyo alikuwa ni mwenye maoni yake tunapokhitilafiana juu ya Hadith ya Mtume (s.a.w.).**63**

Nyingine ni ile iliyopokewa kutoka kwa Anas alisema: "Bilal aliamr-ishwa aadhini na kufuatilizia na iqama."**64** Watu waliopokea ni kama wafuatao: Abu Qalaba na Anas. Suleiman Bin Harb Al-Basri.

Ibn Naafi na Ibn Saad na Yakub bin Shabih na Ibn Kharashi na Nasai na Ibn Hajar wamesema huyo alikuwa ni mtu mkweli.**65**

f) Mwingine ni Hammad bin Zayd bin Dirham. Alisifiwa na Ibnul Mahdi. Na akasema Yahya bin Yahya An-Nasaburi: Amesema Yahya bin Yahya Naisaburi: "Sijaona mtu aliyehifadhi kama yeye."

Amesema Ahmad: Huyo alikuwa ni katika maimamu wa waislamu katika watu wa dini ya kiislamu.

Ibn Hajar naye juu yake amesema: "Alikuwa ni mwaminifu na fakihi thabiti."**66**

Samak bin Atiyya Al Mahdi. Amesema Ibn Mu'in na Nasai: "Huyo alikuwa mwaminifu."**67**

63 *Tahdhibut-Tahdhiib*, Juz. 1, uk. 374

64 *Sahih Bukhari*; Kitabu cha adhana Mlango wa adhana Juz. 1, uk. 314

65 *Rijal Sahih Bukhari* Juz. 1, uk. 314

66 Rejea iliyopita, Juz. 1, uk. 199

67 *Sahih Bukhari*, Juz. 1, uk. 346

Ayyub bin Abi Tamima Sakhtani Al-Anzi: Amesema Ibnul Madani: "Huyo ni katika wa Ibn Sirin, ni mkweli." Pia amesema hivyo Ibn Saad na Abi Khaythama na Nasai."[68]

Ibn Umar alikuwa akisema: "Waislamu walipofika Madina walikuwa wakikusanyika kwa Swala bila ya kuitwa, siku moja wakazungumzia jambo hilo, wengine wakasema: "Wekeni kengele kama ya manaswara, wengine wakataka parapanda kama la mayahudi, Umar akasema kuwe na mtu atakayewaita kwenye Swala, ndipo Mtume (s.a.w.) akaamwambia Bilal: "Simama ee Bilal na uite watu kwenye Swala."[69]

Wapokezi wa hii ni hawa wafuatao:
Mahmud bin Ghaylani Al-Maruzi. Nasai amesema huyu ni mkweli. Pia Muslima amesema hivyo.[70]

Abdur Razzaq bin Hamam bin Naafii Al-Humayri Al-Yamani
Amesema Hisham bin Yusuf: "Abdur Razaq alikuwa ni mwenye ujuzi zaidi na ni mwenye kuhifadhi zaidi miongoni mwetu. Abu Hatami naye amesema: "Hadith zake husajiliwa na hutolewa hoja: na pia Ibnu Habban alimtaja katika kitabu '*Thuqaat*.' Miongoni mwa mafakihi wa watu wa Hijaz. Ibn Hajar naye amesema kumhusu: 'Alikuwa ni mkweli na mwenye Hadith nyingi.

Nafi'i Abu Abdallah (huria wa Ibn Umar)

Amesema Saad: "Alikuwa ni mkweli mwenye Hadith nyingi. Amesema Ibn Khirashi: "Huyo alikuwa ni mkweli."[71]

---

68 Rejea iliyopita, Juz. 1, uk. 81

69 *Fathul Bari* katika *Sharhul Bukhari* Juz. 2, uk. 77 Kitabul adhan, Mlango wa kuanza adhana

70 *Rijal Sahih Bukhari*, Juz. 2, uk. 496

71 *Tahdhiibut-Tahdhiib*; Juz. 2, uk. 746

Baada ya kumaliza juu ya usahihi wa sanad atika riwaya hizi, kwenye upande mmoja, na na kutokuwa sahihi kwa riwaya tulizozitaja kabla yake juu ya mwanzo wa adhana kwa upande mwingine, yafaa kuwe na swali: Nini makusudio ya neno la mpokezi wa Hadith 'Bilal akaamrishwa?'

Ibn Hajar Al-Asqalani anasema katika kujibu hilo: "Neno lake 'akaamrishwa Bilal' hii mara nyingi katika riwaya nyingi ni katika *mafu'uul*, watu wa *Usuul* na watu wa Hadith wamekhitilafiana katika kuifanya tamko hili kwa sigha ya *raf'u*, na hakika ilivyo dhahiri ni kwamba makusudio ya kuamrishwa, katika jambo la kisharia basi ni lazima kumfuata Mtume (s.a.w.)."[72]

Hivyo utaona kuwa Ibn Hajar anaeleza wazi wazi kuwa amri katika ibada inatoka kwa yule mwenye kutoa amri katika mambo ya kiibada na anatilia nguvu hilo kuwa ni lenye kuwafikiwa.

Nami nasema, kama ilivyo katika kuthibitisha jambo la ibada, basi pia inakuwa hivyo hivyo katika jambo la kuanzishwa kwa jambo la kiibada bila ya tofauti yoyote.

Pili, Kauli isemayo kuwa kuanzishwa kwa adhana ni kutokana na ndoto aliyoiota Abdallah bin Zaid inapingana na cheo cha utume na uwekaji sharia nayo inazingatiwa na inakataliwa katika upande huu hali ikiwa kauli hii ina uwiano na nafasi ya unabii wala haipingani na misingi iliyokubaliwa na pande mbili.

Na ama kulingana na waliyoyataja katika kuanzishwa kuwekwa adhana ni ndoto ya Abdalla bin Zaid kwamba Mtume alichukua adhanaa kutoka kwake hilo ni kosa, kulingana na Mtume (s.a.w.w)

72 *Fat'hul Bari* kwa sherhe ya *Sahih Bukhari*, Juz. 2, uk. 8

kama ilivyokuja kutoka kwa Imam Sadiq kuwa hilo ni jambo baya. Ambapo imepokewa kutoka kwake kwamba amewalaani watu wanaodai kuwa Mtume alichukua adhana kutoka kwa Abdallah bin Zaid, akasema: "Umeshuka wahyi kwa Mtume wenu na mwadai kuwa amechukua adhana kutoka kwa Abdallah bin Zaid?"[73]

Tatu: Twaona kuwa Mtume aliweka utaratibu wa kuondoa hitilafu na mikanganyo atakapoondoka, nayo nako ni kurejea kwa Ali na Ahlul-bayt wake ambao wao ndio wajuao zaidi yaliyomo ndani.

Imepokewa kutoka kwa Abu Ayyubul-Answari, amesema, nimemsikia Mtume akisema kumwambia Ammar bin Yasir, "Ewe Ammar, kitakuuwa kikundi kiovu. Nawe uko katika haki, na haki iko pamoja nawe. Ewe Ammar, ukimuona Ali amefuata wangwa na watu wamefuata mwingine, basi mfuate Ali na uwaache watu kwani yeye hatokuongoza kwenye maovu na hatokutoa kwenye uongofu."[74]

Na imepokewa kutoka kwa Aisha kwamba Mtume amesema: "Haki iko pamoja na Ali popote aendapo."

Na Mtume alituamuru tushikane na watu wa nyumba yake katika Hadith ya Thaqalayni, na makusudio ya kushikamana nao ni kuchukua maneno, vitendo na mafunzo yao ya dini.

Kwa hivyo hakuna kinachobaki ila kufuata misimamo ya Ali na Ahlubayt wake, na wao wamesema wazi kuwa kuwekwa adhana ni kutoka kwa Mwenyezi Mungu, hebu angalia nassi zenye kutoa dalili juu ya hilo:

---

73 *Wasa'ilus-Shia*, milango ya adhan na iqama hadith 3

74 *Kanzul-Ummal*: ya Muttaqi Al-Hindi, Juz. 11, uk. 613, *Tarikh Baghdad*, Juz. 13, uk. 186

1. Ameitaja Asqalani kutoka kwa Al-Bazar kutoka kwa Ali (a.s.) amesema: "Alipotaka Mwenyezi Mungu kumfundisha Mtume wake adhana, aliletewa na jibril mnyama aitwaye Buraq, akampanda.[75]

2. Imepokewa kutoka kwa Abi Jafar katika hadith ya Miraj, amesema: "Kisha akamuamrisha Jibril akaadhini na akasema katika adhana yake: "Hayya ala khayril amal" kisha Muhammad akatangulia akawaswalisha watu."[76]

3. Imepokewa kutoka kwa Abi Abdallah amesema: "Wakati Mtume (s.a.w.) alipopelekwa Israi, nilihudhuria Swala na Jibril akaadhini."[77]

4. Imepokewa kutoka kwa Ali bin Ibrahim, kutoka kwa Muhammad bin Isa bin Ubaid kutoka kwa Yunus, kutoka kwa Aban bin Uthman kutoka kwa Ismail Al Ju'ufi, amesema: "Nimemsikia Abu Jafar akisema, adhana na Iqama zina herufi thalathini na tano, akazihisabu moja moja kwa mkono wake, adhana ikiwa na herufi kumi na nane, na iqama herufi kumi na saba.[78] Pia imo katika *Mir'atul-Uqul*.

5. Imepokewa kutoka kwa Muhammad bin Al-Hasan kwa isnad yake, kutoka kwa Husein bin Sa'id, kutoka kwa Fadhalat na Hammad bin Isa, kutoka kwa Muawiya bin Wahab, amesema: "Nilimuuliza Abi Abdallah kutoana na kuongeza maneno ambayo huwa baina ya idhana na iqama. Akasema: "Hayo hatuyajui."

Na ameipokea Saduq kwa isnad yake, kutoka kwa Muawiya bin Wahab mfano wa hiyo.[79]

---

75 *Fathul Bari fi Sharhil-Bukhari*, Juz. 2, uk. 78 Darul Maarifa, Iraq

76 *Wasailus-Shia*: Muhammad Al-Amili, Mlango 19 hadith 2

77 *Wasa'ilus-Shi'a*; uk. 10

78 *Wasa'ilus-Shi'a*; Juz. 5, uk. 413, Mlango wa namna ya kuadhini

79 *Mir'atul-Uqul*; 15:12, Hadith ya 3

Na amepokea Al-Kulaini, kutoka kwa Ali bin Ibrahim, kutoka kwa Isa bin Muhammad bin Isa, kutoka kwa Yunus, kutoka kwa Muawiya bi Wahab kama hiyo.**80**

Na amepokea Ibn Idris katika mwisho wa kitabu 'As-sarair' akinakili kutoka kwenye kitabu cha Muhammad bin Ali bin Mehbub, kutoka kwa Al-Abbas bin Ma'aruf, kutoka kwa Abdallah bin Mughira, kutoka kwa Muawiya bin Wahab mfano wa hiyo.**81**

Pia iko katika '*Mustadrakil-Wasa'il*.'

6. Mlango wa kuwa haisihi kuongeza maneno katika adhanana iqama nayo ni kusema, 'As-swalaatu khayrun minan nawm **الصلاة خير من النوم**

7. Fiqhur-Ridha amesema - baada ya kutaja sehemu za adhana: "Hakuna katika adhana kuongeza wala kurudiarudia, wala hakuna kusema, **الصلاة خير من النوم** *As-swalaatu khayrun munan nawm.*

Imepokewa kutoka kwa Abul Hasan, amesema: "Neno *Aswalaatu khayrun minan nawm*, ni bidaa iliyozushwa na Bani Umayya, hiyo haimo katika asili ya adhana, sio vibaya mtu akitaka kuwaamsha watu kwa ajili ya Swala akitoa wito huo lakini asiufanye kuwa ni katika adhana, kwani sisi hatuoni kuwa ni adhana."

Na imetangulia awali katika kitabu tulichokitaja kuwa, yeye alisema: "Anayetaka kuwaamsha watu kwa ajili ya Swala kabla ya Alfajiri lakini akasema ' **الصلاة خير من النوم** *Aswalaatu khayrun minan nawm* akiukariri, na inapoingia Swala ya Alfajiri ndipo ataadhini."

80 *Al-Kafi*, Juz. 1, uk. 303

81 *Mustatrafatus Sarair*

MUHTASARI WA UTAFITI

Imeonekana kuwa riwaya zilizopokewa na vitabu vya kisunni vinavyoeleza maneno **الصلاة خير من النوم** *Aswalaatu khayrun minan nawm'* na vingine ambavyo havina utajo huu sanad zake zimeanguka, hazikueleza sanad za upande huo. Isitoshe, namna ilivyowekwa adhana - kama zilivyoeleza riwaya hizo- inapingana na misingi maarufu inayotumika katika kuweka hukmu, pia haiafikiani na daraja ya Mtume. Pia tunaona kuwa wapokezi wake ni kumi na wanne na si mmoja. Na upokezi wa Bukhari juu ya suala hili unapingana na wa wengine kwa hivyo riwaya zinasadikisha kuwa riwaya zinazosema juu ya neno '**الصلاة خير من النوم**' ni kuwa hilo ameliongezea Umar bin Khattab siku zake alipokuwa khalifa.

Pia linalotilia nguvu kuzidishwa kwake katika adhana baada ya mjumbe wa Mungu (s.a.w) ni zile hukumu zilizofanywa kuwa ni sheria khususan katika ***Tathwibi*** kwa ndimi za wanavyuoni wa kisunni.

Ama tukirejea kwenye vitabu vya Hadith na fatwa za mafakihi wafuasi wa madhehebu ya Ahlul Bayt, tutakuwa na uhakika kuwa adhana iliyowekwa katika zama za Mtume (s.a.w.) haikuwa na maneno, **الصلاة خير من النوم** Aswalaatu khyrun minanwm.'

Na ina namna yake isiyokuwa ile iliyofanyiwa taswira na riwaya walizozitegemea mafakihi wengine wa kiislamu wasiokuwa wao.

ORODHA YA VITABU VILIVYO CHAPISHWA NA AL-ITRAH FOUNDATION:

1. Qur'an Al-Kariim - Tafsir Al-Kashif Juzuu ya kwanza mpaka kumi na Nane
2. Uharamisho wa Riba
3. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya kwanza
4. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya pili
5. Hekaya za Bahlul
6. Muhanga wa Imamu Husein (A.S.)
7. Mikingamo iliyomzunguka Imamu Ali (A.S.)
8. Hijab vazi Bora
9. Ukweli wa Shia Ithnaashari
10. Madhambi Makuu
11. Mbingu imenikirimu
12. Abdallah Ibn Saba
13. Khadijatul Kubra
14. Utumwa
15. Umakini katika Swala
16. Misingi ya Maarifa
17. Kanuni za Ndoa na maadili ya Familia
18. Bilal wa Afrika
19. Abudharr
20. Usahihi wa Historia ya Uislamu na Waislamu
21. Salman Farsi
22. Ammar Yasir
23. Qur'an na Hadithi
24. Elimu ya Nafsi

25. Yajue Madhehebu ya Shia
26. Ukusanyaji na Uhifadhi wa Qur'an Tukufu
27. Al-Wahda
28. Ponyo kutoka katika Qur'an.
29. Uislamu mfumo kamili wa maisha ya kijamii
30. Mashukio ya Akhera
31. Al Amali
32. Dua Indal Ahlul Bayt
33. Udhuu kwa mujibu wa Kitabu na Sunna.
34. Haki za wanawake katika Uislamu
35. Mwenyeezi Mungu na sifa zake
36. Amateka
37. Nafasi za Ahlul Bayt (a.s)
38. Adhana.
39 Upendo katika Ukristo na Uislamu
40. Nyuma yaho naje kuyoboka
41. Amavu n'amavuko by'ubushiya
42. Kupaka juu ya khofu
43. Kukusanya swala mbili
44. Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara
45. Kuwaongoza vijana wa kizazi kipya
46. Kusujudu juu ya udongo
47. Maulidi.
48. Tarawehe
49. Malumbano baina ya Sunni na Shia
50. Kupunguza swala safarini
51. Kufungua safarini
52. Uadilifu wa Maswahaba

BACK COVER

Kitabu hiki kinazungumzia kuhusu asili ya adhana na jinsi ilivyokuja kwa Mtukufu Mtume. Kuna tofauti za kimapokezi kati ya madhehebu za Kiislamu, hususan Sunni na Shia. Na pia zipo hitilafu miongoni mwa wanavyuoni wenyewe kwa wenyewe ndani ya madhehebu za Kisunni kuhusu suala hili, kama utakavyoona katika kitabu hiki.

Kitu ambacho wamehitalafiana ni maneno: ***as-Salaatu Khayrun Mina 'n-Nawm,*** kwamba ni maneno ya asili ya adhana au yaliongezwa na watu baada ya Mtukufu Mtume kuondoka? Hili ndio suala linalojadiliwa katika kitabu hiki.

Mwandishi wa kitabu hiki amefanya utafiti wa hadithi na matukio ya kihistoria kuhusiana na suala hili, na kutokana na utafiti wake huo anaonesha kwa uwazi kabisa kwamba maneno: Assalaatu khayrun mina'n-naumi, yameongezwa baada ya Mtukufu Mtume (s.a.w.) na kwamba hayana asili katika Adhana na kwamba maneno yenye asili katika adhana ni: *hayya 'alaa khayril - 'amal.*

Madhumuni ya kitabu hiki sio kuleta ugomvi au malumbano na wale wanaoyakubali maneno: Assalaatu khayrun mina'n-naumi, bali ni kuwafahamisha wale wanaoshangaa wanapowasikia Waislamu wengine hawayatamki maneno haya katika adhana yao na badala yake wanatamka maneno: *hayya 'alaa khayril- 'amal.*

Kimetolewa na kuchapishwa na:
Alitrah Foundation
P.O. Box 19701
Dar es Salaam, Tanzania
Simu:+255 22 2110640
Simu/Fax: +255 22 2127555
Email: alitrah@raha.com
Website: www.alitrah.org
Online: www.alitrah.info